**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE**

**Simu**:
Mkuu wa Shule: +255 754 620 212

Shule ya Sekondari Munanila
80 Barabara ya Heri Mission
S.L.P 178
47512 Munanila, BUHIGWE
**KIGOMA**

TAREHE...............

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi:
……………………………………………..
S.L.P ……………………………………..
……………………………………………

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUNANILA HALMASHAURI YA BUHIGWE MKOA WA KIGOMA MWAKA ……………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka………….. na atasoma tahasusi ya CBG/HGK/HKL/HGL/HGFa.

Shule ya Sekondari Munanila ipo umbali wa Kilometa 60 kutoka Kigoma Mjini barabara ya Manyovu na kilometa 45 kutoka Kasulu Mjini barabara ya Manyovu. Usafiri wa basi kutoka Kigoma mjini unapatikana katika kituo cha

mabasi ama kituo kidogo cha **Mwembetogwa** kwa nauli ya shilingi 10,000 tu na kutoka Kasulu mjini usafiri unapatikana stendi kuu ya mabasi ama kituo kidogo cha **Bogwe** kwa nauli ya shilingi 10,000 tu. Wanafunzi wote wanaotokea barabara ya Mwanza, Sengerema, Geita, Nyakanazi, Kakonko, Kibondo, Kasulu wanashauliwa kupanda basi la **'KWA NEEMA TU**' ambalo linatokea Mwanza Jijini hadi Munanila (Manyovu) Centre. Wanafunzi wanaotokea barabara za Tabora ama Sumbawanga wanashauliwa kushukia stendi ya Kigoma Mjini.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ............... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni bila kuchelewa kwa ajili ya kuanza masomo mapema.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare za Shule

(a) Aje na mashati mawili meupe mikono mirefu yenye kola
(b) Aje na suruali mbili nyeusi za kitambaa cha kushonwa zenye marinda
(c) Aje na Viatu vya raba na bukta ya blue kwa ajili ya michezo
(d) Aje na Viatu vyeusi vya ngozi na Soksi nyeusi jozi mbili.
(e) Aje na Kizibao cheusi pamoja na tai nyeusi
(f) Track suti nyeusi kwa ajili ya kusomea usiku au inapatikana jirani na shule kwa shilingi 25,000 tu
(g) Sweta 1 rangi "damu ya mzee" yenye shingo ya "V" au inapatikana jirani na shule kwa shilingi 15,000 tu
(h) Tshirt 1 rangi ya BLUE yenye kola au inapatikana jirani na shule kwa shilingi 15,000 tu
(i) Aje na Tshirt moja ya njano yenye kola kwa ajili ya kazi za jioni na kushindia

### 2.2 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni

(i) Vifaa vya malazi kama chandarua, mto, blanketi, mashuka mawili (blue)
(ii) Vifaa vya chakula kama sahani, kikombe, kijiko n.k
(iii) Aje na godoro dogo la mwanafunzi
(iv) Aje na daftari (counter books) kulingana na tahasusi aliyopangiwa
(v) Karatasi nyeupe (Ream – A4) mbili kwa mwaka
(vi) Mathematical Set, Scientific Calculator, dissecting kit na laboratory coat (CBG)
(vii) Aje na kiti cha plastic rangi nyekundu/blue
(vii) Faili Folder moja la kawaida (la kaki)

(viii) Wanafunzi wote wa HKL, HGK na HGFa waje na **panga** moja na wanafunzi wote wa CBG na HGL waje na **fyekeo** moja kwa ajili ya usafi wa mazingira
(ix) Aje na soft broom moja, mopa moja na ndoo ndogo 2 na sabuni ya maji lita 5

## 2.3 Michango mbalimbali ya shule

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hii ilipwe kupitia Benki ya NMB namba **51401200130** jina la akaunti ni **Munanila Secondary School - Capt.** Fedha hii inasisitizwa kulipwa kwenye akaunti ya shule kuanzia tarehe **01.07.2025** na mwanafunzi afike shuleni na BPS ya Benki na kamwe mwanafunzi asifike na fedha taslimu 'cash' shuleni.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Matokeo ya kidato cha nne (Result slip - copy)
vi. Cheti cha kuzaliwa (copy)

**N.B:**

**Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo**

**mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- Makamu Mkuu wa Shule: : +255 657 591 772<br>+255 763 153 051

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza **kikamilifu.**

**KARIBU SANA!**

**MALONGO, L.A**
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
HULE YA SEKONDARI MUNANILA
P.O.Box 178
ASULU

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE**

**SHULE YA SEKONDARI MUNANILA S.L.P 178 BUHIGWE**

FOMU NA. 1

HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi ………………………………………………………………………………………
2. Jina la baba …………………………………………………………………………………………………..
3. Jina la mama ………………………………………………………………………………………………
4. Jina kamili la mlezi …………………………………………………………………………………
5. Anuani ya mzazi/mlezi ……………………………………………………………………………
6. Uhusiano wa mlezi …………………………………………………………………………………
7. Kazi ya baba/mlezi …………………………………………………………………………………..
8. Kama ni mkulima, zao analolitegemea …………………………………………………………..
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ………………………………………………………..
10. Kama ni mfanyakazi, kazi yake ………………………………………………………………………..
11. Afya ya mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya hivyo kustahili huduma maalum, tafadhari mzazi/mlezi aeleze wazi …………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………………………..
12. Madhehebu ya dini ……………………………………………………………………………………
13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi:

| | Jina kamili | kazi yake | namba ya simu |
|---|---|---|---|
| (a) | ……………………. | ………………… | ……………………… |
| | | | Bandika picha |
| (b) | ……………………. | ………………… | …………………………… |
| | | | Bandika picha |
| (c) | …………………….. | ……………………. | …………………………….. |
| | | | Bandika picha |

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MUNANILA**

FOMU NA. 2

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Jina la mwanafunzi ……………………………………………………………………………….

Jina la mzazi/mlezi ……………………………………………………………………………….

Anuani ya mzazi/mlezi ………………………………………………………………………….

Uhusiano ………………………………………………………………………………………….

Mimi ……………………………………………………………….. nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa Tanzania, naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo naahidi kuwa, nitajibidisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi.

Ili kutimiza shabaha hiyo, **ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa busara, juhudi ya hali ya juu kabisa na kutii kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria.** Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Saini ya mwanafunzi ………………………………………………………. Tarehe …………………….

---

Mimi ………………………………………………… mzazi/mlezi ……………………………………… ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na uongozi wa shule.

Saini ya mzazi/mlezi ………………………………………………… tarehe …………………………..

**BUHIGWE DISTRICT COUNCIL**

**MUNANILA SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 178 BUHIGWE**

FORM NO. 3

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a Medical Officer in respect of all form V entrants)

Student's full name ..........................................................................................
Age… ......................sex.......................................................................................
Blood found (red and white)...............................................................................
Stool examinations...............................................................................................
Urinalysis.................................................................................................................
Syphilis and other.................................................................................................
General Diseases test...........................................................................................
T.B Test.....................................................................................................................
Eye Test....................................................................................................................
Ears Test...................................................................................................................
Chest.........................................................................................................................
Spleen.......................................................................................................................
Abdomen..................................................................................................................
Urine for planet......................................................................................................
Additional information (if any e.g. physical impartment (s) (e.g. arm leg etc) infections chronic or families disease etc.
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
I certify that the above is fit to pursue further Execution on as stated above
Signature..................................................................................................................
Designation..............................................................................................................
Station.......................................................................................................................
Date..........................................................................................................................

**Official Stamp**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE**
**SHULE YA SEKONDARI MUNANILA**

*KIAMBATANISHO "A"*

## RANGI ZA SARE ZA SHULE

1. **SURUALI, KIZIBAO, TAI, TRACK SUIT – RANGI NYEUSI**



2. **SWETA MIKONO MIREFU – RANGI "DAMU YA MZEE"**



3. **T'SHIRT, SHUKA, BUKTA – RANGI YA BLUE**

